



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA



Tarehe. 19.06.2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela anapenda kuwakaribisha Watanzania wote wenye sifa za kuomba nafasi ya kazi ya **Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja II** katika Halmashauri ya Kyela baada ya kupata kibali cha ajira kwa Katibu Mkuu Utumishi Kumbukumbu Namba FA.170/364/01 "B"/63 ya tarehe 14/04/2023.

**1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II NAFASI 1**

**Sifa za mwombaji**

- Awe amehitimu kidato cha nne.
- Awe na Stashahada (NTA Level 6) katika fani ya Urasimu ramani (Cartography) au (Geoinformatics), Sheria, Afya au Masijala kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na wenye ujuzi wa Kompyuta.

**Kazi na Majukumu ya Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II**

- Kuorodhesha barua zinazolingia masijala kwenye rejista (Incoming correspondence register)
- Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi (Outgoing correspondence register)
- Kusambaza majalada kwa Watendaji (Action Officers)
- Kupokea majalada yanayorudi masijala toka kwa Watendaji
- Kutafuta kumbukumbu/ nyaraka/majalada (rack/filing cabinets) au mahali pengine panapohifadhiwa
- Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (File tracking)

**MASHARTI YA UJUMLA**

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usio pungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Mwombaji aambatanishe maelezo yaliyojitosheleza (CV)  
Yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika pamoja na namba zao za simu. Maombi yaambatanishwe na picha moja (Passport size) ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma.
- Barua za maombi ziandikwe kwa mkono na ziambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu kutoka vyuo vinavyotambulikana na Serikali.
- Testimonials provisional results, Statement results hazikubaliki.
- Waombaji wote waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.



- Waombaji wote watapaswa kuangalia mara kwa mara kwenye Tovuti ya Halmashauri kwani wale watakao itwa kwenye mchujo wa awali majina yatawekwa hapo.
- Maombi yatumwe kwa njia ya posta kwa anwani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Kyela,  
S.L.P 320,  
KYELA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **03.07.2023**

Nakala kwa:-

- Katibu Secretariat ya Ajira Katibu katika Utumishi wa Umma  
Jengo la Utumishi (**UDOM**)  
S.L.P 2320,  
**DODOMA.**
- Mbao za Matangazo
- Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya Kyela.



**Kenneth L. Nzilano**

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
KYELA.**

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KYELA

---

Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, S. L. P. 320, Kyela, Mbeya, Simu. 025-2540035/7, Nukshi 025-2540425,